

# BAADHI YA HATUA NA RATIBA ZA KUANDAA MPANGO MADHUBUTI WA KUTOA HUDUMA ZA AFYA WILAYANI

S/No	Shughuli	Muhusika	Kukamilika/Mwisho
1	Halmashauri Taarifiwa au zitakusanya taarifa kuhusu rasilimali zilizopo kutoka vyanzo vya ndani na nje ya wilaya kwa mwaka wa fedha ujao.	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wilaya na Wadau wengine.	Mwishoni mwa mwezi Novemba
<b>Wilaya zinahirikisha wananchi katika zoezi hili?</b>			
2.	Halmashauri au Timu ya Menejimenti ya Afya ya Wilaya itakusanya vipaumbele kutoka Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati, Jamii na wadau wengine Ili kuviingiza Katika Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani.	Halmashauri na Menejimenti ya Afya ya Wilaya	Katikati ya Mwezi wa Desemba
<b>Wananchi mnakumbuka kuulizwa vipaumbele hivi?</b>			
<b>Muda huu wa kukusanya vipaumbele unatosha kwa wilaya nzima?</b>			
<b>Wajumbe wa kamati za vituo vya afya, zahanati na kata wanashiriki katika kukusanya vipaumbele?</b>			
3.	Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani unaandaliwa, ambapo Bodi ya Huduma za Afya ya wilaya inafanya tathimini na kuupitisha Mpango huo.	Timu ya Mipango ya Afya ya Wilaya/ Bodi za Huduma za Afya ya Wilaya	Katikati ya Mwezi Januari
<b>Wananchi wanajua kinachopitishwa?</b>			
<b>Wajumbe wa kamati za vituo vya afya, zahanati na kata wanaidhinisha vipaumbele?</b>			
4.	Kuandaliwa kwa bajeti ya Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani.	Mweka Hazina wa Wilaya/ Afisa Mipango wa Wilaya/ Menejimenti ya Afya ya Wilaya	Mwishoni mwa Mwezi Februari
<b>Wananchi wanashirikishwa katika kuandaa bajeti hii?</b>			
<b>Wajumbe wa kamati za vituo vya afya, zahanati na kata wanashiriki katika kuandaa bajeti hiyo?</b>			

S/No	Shughuli	Muhusika	Kukamilika/Mwisho
5.	Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani pamoja na Bajeti zake zinaingizwa katika Bajeti ya wilaya	Menejimenti ya Afya ya halmashauri	Katikati ya Mwezi Machi
<b>Wananchi wanajulishwa juu ya zoezi hili?</b>			
6	Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani unawasilishwa kwa Sekretariati ya Mkoa ili kuukagua kama unalingana na mwongozo wa Taifa. Mapendekezo yote kutoka kwa Sekretariati ya Mkoa yanawasilishwa kwa maandishi.	Mkurugenzi wa Halmashauri/Sekretarieti ya Mkoa/ Menejimenti ya Afya ya Mkoa	Mwishoni mwa Mwezi Machi
<b>Vipaumbele vinavyokusanywa kutoka kwa wananchi navyo vinakaguliwa?</b>			
7.	Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani pamoja na Bajeti unaidhinishwa na Baraza la Madiwani	Baraza la Madiwani	Wiki ya kwanza ya Mwezi Aprili
<b>Mpango huu unaandaliwa kwa lugha ya Kiingereza. Je, madiwani wote wanajua kiingereza cha Kitaalam?</b>			
<b>Madiwani wanao utaalam wa kuchambua kwa kina yaliyomo kwenye mpango huu?</b>			
<b>Madiwani wanahakiki vipaumbele vya wananchi kutoka kata zao kama vimeingizwa katika Mpango huu?</b>			
<b>Nakala za mpango huu zinafikishwa kwa wananchi?</b>			
8.	Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani pamoja na Bajeti Unawasilishwa kwa Sekretarieti ya Mkoa (nakala 3)	Menejimenti ya Afya ya Halmashauri	Wiki ya Pili ya Mwezi Aprili
9.	Makadirio ya Mpango Madhubuti wa Kutoa Huduma za Afya Wilayani yanatumwa na Katibu wa Mkoa kwenda Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), na nakala yake inatumwa kwa Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii	Sekretarieti ya Mkoa/ Menejimenti ya Afya ya Mkoa	Mwishoni mwa Mwezi Mei

